



Hapo zamani, kulikuwa na
mbuzi aliyeitwa Igobe.
Igobe alikuwa mfalme wa
mifugo na ndege. Aliishi
maisha mazuri.

Siku moja, Igobe aliwaita
mifugo wote na ndege
mkutanoni.




"Rafiki zangu, nimewaita kwa sababu niliota ndoto," Igobe alisema. Mifugo wote na ndege walimsikiliza mfalme wao kwa makini.



"Niliota kuwa kulikuwa na
njaa na ukosefu wa maji
katika nchi yetu. Wengi wa
jamaa zetu walifariki!"
Mfalme alisema.

Mifugo na ndege
waliposikia ndoto ile,
walijawa na hofu.
"Tutafanyaje?" Paka aliuliza.



Kuku na Bata walikuwa na wazo. Walisema, "Kila mmoja wetu alete chakula kiwekwe katika hifadhi ya mfalme."


Mifugo wote na ndege walikubaliana na wazo hilo.



Mfalme alitoa sharti moja.
Alisema, "Yeyote
atakayekosa kuleta chakula,
mtamfunga mumlete
kwangu."



Wakati wa mfalme Mbuzi kustaafu ulifika. Mifugo wote na ndege walikutana kumchagua mfalme mpya. Paka alichaguliwa kuwa mfalme wao mpya.



Mbuzi hakumtambua Paka
kama mfalme. Alisema,
"Mimi ndiye mfalme na
hakuna mwingine. Siwezi
kumtii mwingine yeyote."



Mifugo walipeleka chakula
katika hifadhi ya mfalme
wao mpya. Mbuzi
hakupeleka chochote.


Ng'ombe alisema, "Mbuzi
alipokuwa mfalme, tulimtii.
Hataki sasa kumtii mfalme
wetu mpya. Tufanyeje?"



Mifugo wote na ndege walikasirika. "Kwani anadhani yeye ni tofauti nasi?" Walinung'unika.



Mbwa alisema, "Nilimsaidia
alipokuwa mfalme. Sikuwa
nikilala usiku. Kila wakati
nilikuwa naye, tayari
kumsaidia."



Kondoo alisema, "Nilimpatia
sufu yangu ili awafunike
wanawe."



Nguruwe naye alisema,
"Alipokuwa mfalme,
aliwaambia marafiki zake
kuwa mimi ni mlafi. Lakini
nilitumia muda mwingi
kuitunza bustani yake na
kupalilia mawele na
mahindi."



Kondoo aliuliza, "Eti alisema nini? Kwamba wewe ni mlafi? Alifikiri kuwa atakuwa mfalme milele?" Kondoo aliongeza kusema, "Lazima afahamu kuwa yeye si mfalme tena. Hata sijui kwa nini anafikiri kuwa yeye ni muhimu sana."




Mifugo wote walicheka na kukubaliana kwamba lazima Mbuzi apeleke chakula kwa mfalme mpya. Mfalme Paka alimwamuru Mbuzi aende kwake.



Mifugo walipoenda,
walimkuta Mbuzi
akistarehe. "Siendi kwa
Paka. Hakuna mfalme
mwingine ila mimi. Ukiwa
mfalme, unasalia mflame."
Mbuzi alisema kwa kiburi.



"Basi tutakufunga kwa
kamba tukupeleke kwa
mfalme mpya," Kondoo
alisema.



Ng'ombe alimfunga Mbuzi akamvuta na kumpeleka kwa mfalme. Kondoo, Bata, Mbwa, Nguruwe na Jogoo walimshangilia Ng'ombe wakisema, "Mpeleke huyu mbuzi kaidi kwa mfalme mpya!"

Tangu wakati huo, kila mbuzi hukataa kusonga anapovutwa.
Hufikiri kuwa anapelekwa kwenye mahakama ya mfalme.



